

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi
Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.
Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

WAZIRI JAFFO AMMWAGIA SIFA RC MAKONDA KWA KUWAJALI WALIMU.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa TAMISEMI Mhe. Suleiman Jaffo ameupongeza Uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kupitia Jitihada binafsi za Mkuu wa mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda kwa kuwaboreshea Walimu mazingira ya kazi ikiwemo ujenzi wa ofisi 402 za walimu.

Waziri Jaffo ametoa pongezi hizo wakati wa hafla ya uzinduzi wa Pikipiki 2,894 zenye thamani ya zaidi ya shilling Billion 8.5 zilizotolewa kwa waratibu wa elimu Kata ambapo kitaifa Zoezi hilo limefanyika Dar es salaam.

RC Makonda amesema anajivunia kuona Dar es salaam inaendelea kushika kidedea kwenye matokeo ya mitihani ya kitafa kutokana na walimu kuwekewa mazingira bora ya kazi ikiwemo ujenzi wa ofisi 402 za kisasa za walimu, mikopo ya viwanja vya bei nafuu pamoja na kusafiri Bure kwenye daladala na Treni ambapo amesema bado ipo mipango mingi ya kuhakikisha walimu wake wanaishi vizuri ili wawe na motisha ya kazi.

Aidha RC Makonda amesema pikipiki zilizotolewa zitaenda kuongeza nguvu na hari ya kazi kwa waratibu wa elimu Kata ambapo kwa mkoa wa Dar es salaam umepata pikipiki kwa kila Kata.

Pikipiki 2,894 zilizotolewa kwa waratibu wa elimu Kata nchi nzima zimenunuliwa na wizara ya elimu na wafadhili kutoka Global Partnership in education kwa lengo la kuwawezesha kuzitembelea shule kwenye Kata zao ili kuboresha elimu.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

04/07/2018